Jina…….. Nambari Yako…….

102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2
(LUGHA)
Julai/Agosti 2013
Muda: Saa:2½

Sahihi ……

Tarehe……

MTIHANI WA MWIGO – WILAYA YA KIHARU/KAHURO
KIDATO CHA NNE - 2013

Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
KISWAHILI
Karatasi ya 2
(LUGHA)
Muda: Saa:2½

MAAGIZO:
1. Karatasi hii ina maswali manne (Ufahamu, Ufupisho, Lugha na Isimu Jamii).
2. Jibu maswali yote kwenye nafasi zilizoachwa baada ya kila swali.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

	SWALI	UPEO	Alama
1	Ufahamu	15	
2	Ufupisho	15	
3	Matumizi ya Lugha	40	
4	Isimu Jamii	10	
	JUMLA	80	

1. **SEHEMU A: UFAHAMU**

Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali.

Kuna nuru nyingine ambazo huzimwa mapema kabla ya kuangaza ipasavyo kama ilivyokuwa ya mwandishi Katama Mkangi. Katama Mkangi alikuwa Mkenya halisi aliyetetea kupatikana kwa uhuru wa kila mtu.

Wakati huo, watu wengi walikuwa wanaogopa kushughulikia ama kuyazungumzia masuala haya kwa sababu ya hali ya kisiasa ilyokuwepo wakati huo.

Uhuru wa kusema ulikuwa duni na watu wengi waliogopa kuhujumiwa kwa kuikosoa serikali. Hayo hayakumzuia Mkangi kuzikosoa sera za serikali zilizowaumiza raia wengi na kuwakosesha uhuru wao.

Kwa sababu hiyo, mwandishi huyu alitiwa kizuizini mwaka wa 1986. Serikali ya wakati huo ilitetea kifungo chake ikidai kuwa alihusika na kikundi cha chini kwa chini kilichojulikana kama *Mwakenya* ambacho kilisemekana kilitaka kuangusha serikali. Hata hivyo, watu wengi nchini Kenya waliamini kuwa kushikwa kwake kulitokana na msimamo wake ambao ulipinga utawala uliokuwepo.

Baada ya kutoka kizuizini alinyimwa kazi katika vyuo vikuu vya umma kutokana na msimamo wake kuhusu maswala ya kiutawala na sera za serikali ambazo alizipinga.

Mwandishi huya ameandika kazi za kifasihi nyingi. Kando na *Walenisi*, riwaya zake nyingine ni *Ukiwa* (1975) na *Mafuta* (1985). Pia, ameandika hadithi za watoto kama vile *Matunda Sita Mtini*.

Katika riwaya yake ya Ukiwa, Mkangi anamulika matatizo yanayowakumba vijana wa kike na kiume. Anatalii matatizo yanayowanasa vijana hasa kutoka vijijini wanapoenda katika miji wanakopatwa na majonzi na ukiwa mwingi.

Riwaya ya *Mafuta* inashughulikia masuala ya ukoloni mamboleo na mateso yanayowapata raia wa kawaida chini ya mfumo wa ubepari. Anasema Mkangi kuwa ubaguzi na ukabila unazaa njaa, chuki, uchafu, magonjwa na kila aina ya dhiki kwa maskini huku matajiri wakiishi katika fahari kuu.

Napo katika riwaya ya Walenisi, mwandishi anamulika shida zinazotokana na uongozi mbaya na sera ambazo haziwaendelezi watu na utu kwa jumla katika jamii. Tabaka la wachache, linaloongoza kwa ujanja na kimiliki njia za kuzalisha mali, linakaa na kuishi raha mustarehe huku walio wengi wakitaabika na maisha duni licha ya kufanyishwa kazi. Wanawapendelea walio wachache na kuwakanadamiza walio wengi kwa kukosa utu.

Hii ndio sababu nchi ya Walenisi tunayomulikiwa ni ulimwengu uliofikia kiwango cha juu sana cha maendeleo na ufanisi kwa sababu ya sera zake nzuri – kuheshimu haki za watu, kufuata sheria na katiba iliyowekwa na kujali hali za walio wengi kwa kusambaza raslimali zake kwa umma kwa usawa.

Riwaya ya *Walenisi* inamulika maswala ya kijamii. Mkangi anahoji kuwa mfumo ambao jamii inachukua kuongoza maendeleo yake ni muhimu sana katika kufikia maendeleo fulani katika jamii ama kutoyafikia na hivyo kuzuka kwa matatizo katika jamii husika. Je, ni mfumo upi ufaao katika kuendeleza utu na kuwajenga wanadamu wakamilifu katika jamii? Hili ni swali ambalo mwandishi analishughulikia kwa mapana na marefu.

Kulingana na Mkangi hili linawezekana tu ikiwa uongozi ambao uko katika jamii yoyote utakuwa wenye kujali maslahi ya wote bali si kujijali wenyewe na kujilimbikizia mali huku walio wengi wakiwa wanalala njaa.

Kiswahili Karatasi ya Pili *2*

MASWALI

(a) Taja vitabu **vinne** alivyoandika Mkangi.. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(b) Kwa nini Mkangi anasemekana kuwa nuru? (alama 4)

_____

_____

_____

_____

(c) Toa sifa **tatu** za Mkangi kama zinavyoelezwa. (alama 3)

_____

_____

_____

_____

(d) Eleza maudhui matatu katika kazi za Mkangi. (alama 3)

_____

_____

_____

_____

(e) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa kwenye ufahamu. (alama 3)

(i) Nyeti _____

(ii) Ubepari _____

(iii) Duni _____

2. **SEHEMU B: UFUPISHO**

Soma taarifa ituatayo kasha ujibu maswali

Kuna mambo kadha ambayo yamejitokeza hivi majuzi yanayonitia wahaka kuhusu kuundwa katiba ya aushi na ya kudumu. Mosi, kuna watu ambao wanachukulia kuwa lazima tuunde katiba itakayolinda maslahi ya wanasiasa walioko sasa. Katika uundaji wa afisi mbalimbali wanafikiria maslahi ya watu wa makabila yao wala si asasi zinazohusika. Fikra hizi ndizo zilizowafanya watu kuandamana mitaani, wakiwahimiza wajumbe kuhakikisha kuwa tuna afisi maalum zilizotengewa watu Fulani. Licha ya heshima tuliyonayo kwa viongozi wetu wa sasa, si sawa kuunda afisi kwa ajili yao. Tuunde afisi kwa sababu zinahitajika kwa maendeleo ya nchi yetu na zinalinda maslahi ya kila mwananchi. Tujitahidi kupunguza imani za kikabila katika kuunda sheria hii kuu. Tuongozwe na fikira za kizalendo, fikira za kujenga taifa moja kupitia lugha ya Kiswahili.

Pili, kuna watu ambao kutokana na shinikizo za mataifa ya nje, wanataka tuwe na katiba itakayolinda haki za wageni kuliko za wananchi. Jambo hili linasikitisha sana. Sheria hii kuu ni mali ya Wakenya na ndio wanapaswa kuiongoza na kufikisha hatima yake. Kama ijulikanavyo na wengi, katiba ni nyenzo ya kuleta maendeleo na kudumisha maelewano baina ya viongozi na wananchi. Ni mkataba baina ya mwananchi mmoja na mwenziwe kuhusu namna watakavyoishi pamoja. Masharti yanayoiongoza serikali ni muhimu yawe kwa manufaa ya mwananchi, hayapaswi kukinzana na haki za mwananchi.

Katiba nyingi za ulimwengu zina kitangulizi kinachoonyesha kwamba katiba ni mali ya taifa na ndiyo sheria kuu nchini. Aidha huonyesha kuwa wananchi wanaafikiana kuwa ndiyo katiba yao na kwamba kuna masharti na maadili ya kimsingi yanayoiongoza. Kwa mfano, ni nchi moja ya kidemokrasia? Ni nchi iliyopunguza na kusambaza madaraka mashinani? Je, inaamini katika heshima, usawa na haki kwa wananchi wote? Kuna imani yoyote kuhusu uraia, wimbo wa taifa, bendera ya taifa na lugha ya taifa?

Kitangulizi cha katiba ni mwongozo wa falsafa ya taifa na kinaashiria maafikiano baina ya wananchi kuhusu falsafa hiyo. Wanasiasa wanaochukua hatamu za uongozi wa serikali wanatarajiwa kufuata imani na maelekezo ya kitangulizi hicho cha katiba.

MASWALI

(a) Dondoa mawazo makuu kwa majibu wa aya ya kwanza na ya pili.
(Maneno 80 – 90). (alama 7)
Matayarisho (Mtiririko 1)

Jibu

(b) Ukirejelea aya za mwisho mbili, eleza umuhimu wa kitangulizi cha katiba.
(Maneno 35 – 40). (alama 6)
Matayarisho (Mtiririko 1)

Jibu

_____

_____

_____

3. **SEHEMU C: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA**

A Taja ala za kutamkia zinazotumiwa kuelezea sifa za vokali yoyote ile. (alama 2)

_____

_____

B Nomino hizi hupatikana katika ngeli zipi? (alama 2)

(i) Vita _____

(ii) Dunia _____

C Kitenzi pakata kiko katika kauli ipi? (alama 1)

_____

D Andika sentensi ifuatayo katika **usemi** wa **taarifa**. (alama 3)

"Mimi nitawakaribisha wageni leo jioni. Kisha nitaondoka kwenda kwangu kesho." Fatuma alimwambia Juma.

_____

_____

_____

E Tofautisha kati ya: (alama 2)

(i) Ungesoma kwa bidii ungepita mtihani.

_____

_____

(ii) Ungalisoma kwa bidii ungalipita mtihani.

_____

_____

F Bainisha matumizi ya **'KI'** katika sentensi zifuatazo. (alama 2)

(i) Kizee hiki kilinichezea kijinga.

_____

(ii) Akimpenda atamkirimu.

_____

G Pigia mstari viunganishi kwenye sentensi zifuatazo kisha ueleze ni vya aina gani. (alama 2)

(i) Aliniadhibu ilhali sikuwa na hatia.

_____

(ii) Usijaribu kumpunja kwa ajili ya kutojua kusoma kwake.

_____

H Andika **kinyume** cha sentensi hii. (alama 1)

(i) Babu alikashifiwa kwa vitendo vyake.

_____

I Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya jedwali. (alama 4)

(i) Ingawa wachezaji wamewasili wakereketwa hawashangilii.

_____

_____

_____

_____

J Tumia neno **'mle'** kwenye sentensi kama: (alama 4)

(i) Kivumishi _____

(ii) Kitenzi _____

(iii) Kiwakilishi _____

(iv) Kielezi _____

K Onyesha mahali panapowekwa **Shadda** kwenye kitenzi katika sentensi ifuatayo: (alama 1)

(i) Kiberiti ki juu ya meza.

_____

L Fafanua maana ya kirai, kisha utunge sentensi sahihi ambayo haina nomino kuonyesha kirai nomino.

_____

_____

M Eleza maana ya dhana ya chagizo kisha uonyeshe kwa kupigia mstari chagizo katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

(i) Mtoto alitembea asteaste.

_____

_____

N Andika kwa **ukubwa**. (alama 2)

(i) Kiti kilichokuwa kimekaliwa na mwanamke kilivunjika.

_____

_____

O Eleza maana zozote tatu zinazopatikana kwenye sentensi hii: (alama 3)

(i) Alikuwa amenijuza kuwa angefika kwao.

_____

_____

_____

_____

P Unda **nomino** kutokana na kitenzi Konga. (alama 1)

_____

_____

_____

Q Yakinisha sentensi ifuatayo ikiwa katika hali ya umoja. (alama 2)

Nyuzi sizingekatika sizingepotea.

_____

_____

R Bainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Mwita alimtumia babake barua kwa posta.

_____

S Tumia kirejeshi **-O-** tamati katika sentensi ifuatayo. (alama 1)

(i) Kijana ambaye anapendendeza ni yule ambaye hutia bidii.

4. **SEHEMU D: ISIMU JAMII**

(a) Tofautisha kati ya lafudhi na lahaja. (alama 2)

(b) Taja aina zozote **tatu** za lahaja. (alama 3)

(c) Eleza sifa tano za lugha ya magazetini. (alama 5)

Kiswahili Karatasi ya Pili *9*

ANSWERS:
Order a copy of answers from www.schoolsnetkenya.com/order-e-copy
NB> We charge Kshs. 100 ONLY to meet website, e-resource compilation and provision costs